KILEMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES

SCHOOL OF MEDICAL LABORATORY TECHNOLOGY

P.O.BOX 19

MARANGU KILIMANJARO

Email:kilemacollegecohs@gmail.com: Website:kilemacollege.ac.tz.

Tel:0712461808 or 0754-461325

Ref:No KICOHS/FULL REG/NO/HAS/129P

To……

P.o. Box ……

Dear Sir/Madam.

YAH: FOMUZA KUJIUNGA NA KOZI YA CHUO CHA MAABARA YA AFYA KILEMA:

Napenda kuichukua nafasi hii kukupongeza na kukuarifu kwamba NACTE(NATIONAL COUNCIL FOR TECHNICAL EDUCATION) wakishirikiana na WIZARA YA AFYA imekuchagua kujiunga na mafunzo ya Medical Laboratory sciences, ngazi ya astashahada/Shahada Kilema College of Health Sciences,kilichopo Kilema-Marangu,Kilimanjaro.

Mafunzo haya ni ya miaka 2kwa wale wa astashahada na miaka3 kwa wale wa shahada.

Masomo yataanza mwezi waApril 2017-tarehe-**24/APRIL/2016**Kwa maelekezo haya ,unatakiwa kuripoti Chuoni mapema kabla ya masomo kuanza.endapo hautafika katika kipindi cha wiki mbili baada ya masomo kuanza hutapokelewa tena.

Kwa hivyo endapo utakuwa bado una nia ya kujiunga na mafunzo yaliyoainishwa hapo juu, itabidi kuomba nafasi upya mwaka wa masomo ufuatao.Au October 2017.

GHARAMA ZA CHUO:

Gharama za Chuo zinafuata utaratibu wa uchangiaji ambao hutolewa kila mwaka kuendana na gharama za uchumi wa nchi unavyokwenda.

JEDWALI LA GHARAMA ZA CHUO:

S/N	MAELEZO	MUHULA WA KWANZA	MUHULA WA PILI
1	ADA YA MASOMO	800,000/=	800,000/=
2	GHARAMA ZA MTIHANI MMOJA	100,000/=	
3	MALAZI KWENYE MABWENI YA CHUO-KILEMA HOSPITALI-KWA MWAKA	300,000/=	00.00
5	CHAKULA	600,000/=	200,000/=
		1800,000/=	1,000,000/=
		JUMLA YA ADA	2,800,000/=

GHARAMA NYINGINE AMBAZO HAZIEPUKIKI NI KAMA ZILIVYO ORODHESHWA HAPA CHINI KWA MWAKA WA KWANZA:

NO	MAELEZO	KIASI
1	KUJISAJILI NACTE	15,000/=
2	MAHAFALI	80,000/=
3	REAM PAPERS)	40,000/=
4	CHAMA CHA WANACHUO.	10,000/=
5	FEDHA ZA TAHADHARI.	20,000/=
6	BIMA YA AFYA-ICHF	30,000/=
7	MAENDELEZI YA CHUO.	50,000/=
8	VITAMBULISHO	10,000/=
9	PROCEDURE BOOKS AND PRACTICUM GUIDES.	50,000/=
10	KEMIKALI NA VIFAA VYA MAABARA(LAB CONSUMABLES).	50,000/=
11	ADA YA MTIHANI WA KUMALIZA	150,000/=
12	T-SHIRT YENYE NEMBO	25,000/=
	JUMLA TZ.SHS	530,000/=

Fedha za mitihani pamoja na za Usajili Nactezinatakiwa uje nazo cash hapa chuoni kwani Wizara ya Afya imeangiza.zibenkiwe kwa pamoja na list ya wanafunzi wanaofanya mitihani ya mwisho wa mwaka Pamoja na vyeti vyao viambatanishwe.

Inasisitizwa kwamba ni fedha ya mitihani na ya kujisajili Nacte pekee ndiyo utakuja nazo hapa chuoni,Fedha nyingine zote zitalipiwa kwenye akaunti ya Kilema College of Health Sciences.

NMB-NELSON MANDELA MOSHI AKAUNTI NO(**40310018728)**-JINA KILEMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES-AU(KICOHS) kwa kifupi.----Au Tawi lolote lile la NMB-NCHINI KOTE.Mwanachuo mtarajiwa anatakiwa siku ya kuripoti chuoni aje na bank-pay-in slip.

Ieleweke kwamba gharama za matibabu zitatolewa kwa wale ambao hawana Bima ya Afya ,ili kuwawezesha kujiunga na Mfuko huu wakati wote watakapokuwa chuoni.Hivyo jumla ya fedha ya uchangia itakusanywa na Mhasibu wa Chuo na kuwasilisha kwa Mratibu wa Bima ya Afya wa Kanda, ambaye atafanya utaratibu na kutoa kadi za Bima ya Afya kwa wanafunzi waliochangia tu.Kwa wale wanafunzi wenye Bima za Afya watakuja nazo chuoni na watakuwa wakitibiwa nazo.

Kabla hujaenda Chuoni hakikisha umepima afya yako kwa Daktari ambaye atajaza fomu iliyoambatanishwa na barua hii.Fomu hiyo utaikabidhi kwa Mkuu wa Chuo mara tu ufikapo chuoni.Wakati wote utakapokuwa chuoni unatakiwa kutii SHERIA NA TARATIBU ZA NCHI, WIZARA YA AFYA PAMOJA NA ZA CHUO HUSIKA.Vile vile ieleweke kwamba masuala yote ya mwanafunzi anapokuwa chuoni yatashughulikiwa na Uongozi wa Chuo, na endapo itakuwa lazima suala la mwanafunzi lishughulikiwa na Bodi ya Chuo au Makao Makuu ya Wizara kupitia Idara ya Mafunzo,basi maombi au matatizo yote yapitie kwa Mkuu wa Chuo kabla ya kuwasilishwa Wizarani.

Usafiri wa kwenda na kurudi chuoni ni gharama ya mwanafunzi na wala si jukumu la Chuo .Hakikisha unakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi yako madogo madogo kwa kipindi chote utakapokuwa chuoni.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja chuoni na vifaa vifuatavyo:

1.Vyeti /Cheti halisi cha kuhitimu elimu ya Sekondari kinachotolewa na Baraza la Mtihani la Taifa.Hakuna mwanafunzi atakayepokelewa chuoni bila kuwa nacheti halisi. Ukibainika kuwa na cheti chochote cha kughushi,utaachishwa masomo na kushitakiwa kwa mujibu wa sheria na chuo hakitawajibika kukurudishia gharama yoyote ikiwa ni pamoja na gharama ya uchangiaji.

2.SARE YA CHUO:

Mwanachuo wa kike:

1Magauni mawili (2) ya tetron nzito nyeupe,yenye mikono mifupi.Hakikisha magauni yanavuka magoti –inch 2 chini ya goti ,isiwe na mpasuo nyuma.Mshono wake ni uwe sawa na sare za wauguzi na iwekwe utepe wa khaki mabegani.viatu vyeupe, vyeusi au kahawia vyenye visingino vifupi.

Mwanachuo wa kiume:

Suruali mbili (2) za rangi ya khaki na mashati mawili yenye rangi nyeupe mikono mifupi na mirefu.

KWA WOTE:

Makoti mawili (2) meupe na masafi yaliyoshonwa kwa tetron nzito nyeupe koti moja liwe na mikono mifupi nala pili liwe na mikono mirefu.

- ✓ Mwavuli.
- ✓ Six counter books-3 quire. And ball point pens.
- ✓ Jaketi au pullover la baridi.
- ✓ A Blanket 1.
- ✓ Shuka mpya 2.
- ✓ Mto 1 na foronya 2-
- ✓ Box files-2
- ✓ Ruler/pencils/stapler
- ✓ Picha Passport size -3 kwa ajili ya kitambulisho
- ✓ Taulo wa wavulana/khanga kwa wasichana
- ✓ Taa /Tochi ya solar kwa tahadhari umeme ukatikapo ghafla.
- ✓ Nguo za michezo
- ✓ Ndoo ndogo ya kuogea ,kufulia na kopo la kuongea.
- ✓ Cheti halali cha ufaulu wa Form 4, leaving certificate na cheti cha kuzaliwa[birth Certificate].

SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO:

1. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa katika eneo la CHUO/MABWENIl ifikapo saa 1.00 jioni siku za kawaida na saa 2.00 usiku siku za mwisho wa wiki na sikukuu .Wanachuo watakaokuwannje ya Chuo/Bweni zaidi ya muda uliotajwa hapo juu kwa sababu maalumu atatakiwa kupata kibali maalumu kwa maandishi (Gate pass)kutoka kwa Mkuu wa Chuo au Mlezi wa Chuo.
2. Kila mwanachuo atawajibika kufanyausafi wa chumba anachoishi na usafi wa mazingira ya Chuo.Hairuhusiwi kubandika magazeti/vipande vyaau picha kwenye kuta za majengo ya chuo.
3. Kila mwanachuo atatakiwa kushiriki kikamilifu katika michezo na shughuli nyingine za chuo kama zitakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
4. Wageni hawaruhusiwi kuingia kwenye vyumba vya wanachuo.Endapo mgeni/wageni watahitaji kuzunguka na kuangalia maeneoya chuo, watatakiwa kupata kibali toka kwa Mkuu/Mlezi wa Chuo.
5. Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanachuo wakati wa vipindi na wanatakiwa kuwa wameondoka kwenye maeneo ya chuo ifikapo saa 12. Jioni.
6. Wageni wanatakiwa kuandikisha katika kitabu cha wageni,kinachoonyesha jina la mgeni,mahali anakotoka ,uhusiano na mwanachuo anayemtembelea, anuani yake na muda wa kuingia na kutoka.
7. Hairuhusiwi wanachuowa kiume kwenda kwenye vyumba vya wanachuo wa kike na vivyo hivyo kwa wanachuo wa kike kwenda kwenye vyumba vya wanachuo wa kiume.
8. Wanachuo wanatakiwa kuvaa sare za chuo wakati wote wanapokuwa darasani ,katika mafunzo kwa vitendo hospitalini na shughuli nyingine za chuo kama itakavyoelekezwa na uongozi wa chuo.
9. Wanachuo wote,wanatakiwa kuvaa koti jeupe na safi wakati wote anapokuwa katika mafunzo kwa vitendo au zamu hospitalini na maabara.

10.Wanachuo wanatakiwa kuvaa nguo za heshima na hadhi wakati wote wanapokuwa chuoni au wanapokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo hospitalini.Zingatia waraka wa mavazi uliotolewa na Idara kuu ya Utumishi mwaka 2011.

13.Wanachuo wote watawajibika kutunza vifaa na majengo ya chuo. Ni marufuku kujihusisha na uharibifu wa aina yeyote .Aidha ,mwanachuo atakayeharibu mali ya chuo,atawajibika kuilipa pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

14.Hairuhusiwa kukaa na silaha ya aina yeyote,ikiwemo kisu ua panga mahali popote chuoni.

15.Mwanachuo akiugua anatakiwa atoe taarifa mara moja kwa Mkuu/Mlezi wa chuo.Kila mwanachuo anayehudhuria matibabu awe na sick-sheet kabla ya kupata matibabu.Isipokuwa pale tu matibabu yake yanakuwa ya dharura na upatikanaji wa sick-sheet ni mgumu.Hata hivyo ,bado mwanachuo huyo atatakiwa kujaziwa sick-sheet baada ya matibabu .Sick-sheet zote zinatakiwa zirudishwe kwa Mkuu/Mlezi wa chuo na kutunzwa kwenye majalada ya kumbukumbu za wanachuo husika.

16.Mwanachuo haruhusiwi kushiriki katika kutenda makosa ya jinai .Aidha mwanafunzi yeyote atakayethibitika kushiriki kutenda kosa ya jinai atasitishwa masomo na kuamuriwa kuondoka eneo la chuo haraka iwezekanavyo.

17.Mwanachuoanatakiwa kushiriki kikamilifu katika matukio yote yanayohusu mafunzo bila kukosa.Ni marufuku kwa mwanachuo kuondoka eneo la chuo/mafunzo bila taarifaya maandishi kutoka kwa mkuu wa chuo/Mlezi wa wanafunzi.

18.Mwanachuoharuhusiwi kutumia lugha ya matusi au udhalilishaji, kupigana ,kufanya migomo au maandamano bila kufuata utaratibu,kuiba na kumiliki mali kinyume cha sheria.

19.Mwanachuo haruhusiwa kufanya vitendo vyenye kushawishi ngono ndani ya majengo ya chuo au hospitali.

20.Mwanachuo anaruhusiwa kushiriki hafla za kiimani zinazohusiana na imani ya dini mbalimbali baada ya kuwa amepata kibali kutoka kwa Mkuu wa chuo .Aidha ,Ushiriki wa shughuli yoyote ya kidini itakayothibitika kuingilia ratiba ya mafunzo au uvunjifu wa amani hautaruhusiwa.

21.Mwanachuo haruhusiwi kushiriki au kuendesha harakati za kisiasa chuoni.

23.Mwanachuo wa kike atakayedhihirika kuwa na mimba au amempa mwanafunzi mwenzie mimba basi atarudishwa nyumbani kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

24.Mwanachuo anatakiwa kufuata taratibu zote wakati wa mitihani.Aidha kushiriki katika kugushi matokeo ya mitihani, nyaraka za serikali hakutavumiliwa.

ANGALIZO:Uvunjaji wa taratibu zilizoainishwa hapa juu unaendana na adhabu ,ambazo zimeelekezwa katika kitabu cha maadili ya wanachuo walioko katika vyuo vya afya kilichotolewa na Wizara ya Afya mwaka 2004

(DISPLINARY CODE FOR STUDENTS IN HEALTH TRAINING INSTITUTIONS, REVISED 2004).

MAULIDI MARAWI.

MKUU WA CHUO.

COLLEGE CAMPUS:

The Kilema College of Health Sciences,School of Medical Laboratory Technology iko mkoani Moshi Kilimanjaro .ukija fika stand ya mabasi madogo ya moshi mjini uliza magari ya marangu kilema nauli halali 2000/= waambie wakushushe barabara ya kwenda Hospitalini Kilema .ukifika hapo kuna usafiri wa taxi 3000/= au bodaboda kwa 1000/=tu utatukuta tupo ndani ya hospital ya kilema .

Barua ya kujiunga na masomo ya Maabara ya Afya ngazi ya Astashahada

KILEMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES 2016/2017.

from Marangu Mtoni to Kilema Hospital .Roads are all- weather passable and transport is abundant.

WELLCOME TO KILIMANJARO AND ENJOY OUR SERENE CLIMATE.

KILEMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES

SCHOOL OF MEDICAL LABORATORY TECHNOLOGY.

P.O.BOX. 19.MARANGU -KILIMANJARO

Email-kilemacollegecohs@gmail.web:kilemacollege.ac.tz.

MEDICAL CERTIFICATE

First Name……Second Name……..Surname……...

Age……..Sex…….Martial Status……Citizenship……...

PERSONAL HISTORY

Is the examinee suffering from any the following? Indicate YES or NO

Tuberculosis…….Pneumonia……Rheumatic Fever…….Allergy……..Diabetes……...

Gastric or duodenal…….Jaundice……Recurrent indigestion…….Dysentery…….

Varicose Veins……Kidney or Urinary disease…….Epilepsy……..Ear…….

Deformity……Psychotic……Eye disorder……Nose or Throat disorder……..

Skin disease……..Anemia……Gynecological disorder……Serious accidents…….

Malaria or other tropical disease……..Major or Minor operations……

Any other serious disorder…….

PHYSICAL EXAMINATION

Skin disease……..Eye Conjunctivae Pupils…….Vision: Right…….Left……

Please state condition of Ears (if any discharge)…….

Mouth and throat……Nose…….any Abnormality……..

Cardiovascular System

Heart Disease…….Blood Pressure Systolic……..Diastolic……..

Heart : Any Murmur?.....Arteries and Veins……..

Abdomen:
Hernia…….Masses…….Liver……Hydrocele……

Any Clinical evidence of hyperacidity or gastric duodenal ulcer?.....

LABORATORY.

Urine Albinum…….Sugar…….Bilharzia…….

Stool: Special emphasis on Hookworm or Bilharzia.

Blood examination: Hb level……

(a) Neuotrophils……..

(b) Eusinophils…….

(c) Lymphocytes……

(d) Monocytes……..

(e) ESR……...

X-Ray Examination –Chest……

Serology: VDRL…….

Pregnancy Test……...

CONCLUSION

I have examined Mr/Mrs/Miss/Sr/Br/……..

That He is/She is not physical and mentally fit to be admitted to higher Studies……..

Name…….Signature……Date…….

Title Qualifications……..

Name of Hospital…….

Stamp……..